UTANGULIZI WA MASOMO YA BIBLIA

SEHEMU YA KWANZA

Masomo haya yameandaliwa ili kutoa elimu ya mafundisho ya msingi wa Biblia kama yalivyo katika Injili ya Yohana kitabu cha nne cha Agano Jipya.

1. (Yohana 6:67-69) Yesu alikuwa nani kwa mawazo ya Petro katika mstari wa 69? _____
2. (Yohana 1:29) Yesu aliitwaje? _____

   Nyakati za Agano la Kale Mungu alitaka Mwana kondoo asiye na ila au waa (doa) atolewe dhabihu ya kuteketezwa kwa ajili ya dhambi za wanadamu. Hii ilikuwa ishara au mfano wa mwana kondoo wa kweli wa Mungu (Yesu Kristo), asiyekuwa na dhambi, aliyekuja kufa kwa ajili yetu sisi wenye dhambi.
3. (Yohana 3:16) Mungu alifanya nini kutokana na upendo wake mkubwa kwa wanadamu? _____

   _____
4. (Yohana 3:16) Ni mambo gani yanayotajwa kuhusu kila aaminiye katika Mwana wa Mungu? _____

   _____
5. (Yohana 3:18) Mungu anasema nini kwa mtu asiyeamini katika Mwana wa Mungu? _____

   _____
6. (Yohana 1:10-11) Je, ulimwengu ulimjua Kristo na kumpokea? Ndiyo / Hapana
7. (Yohana 5:23*)* Asiyemheshimu Mwana wa Mungu hamheshimu nani? _____
8. (Yohana 1:12) Tunakuwa nini mara tunapompokea Kristo na kuliamini Jina lake? _____
9. (Yohana 4:42) Wale waliomwamini walimwitaje Kristo? _____

   "Huu ni usemi wa kiimani na wa thamani kwa wote wanaompokea Yesu Kristo, kwamba alikuja ulimwenguni kuwaokoa wenye dhambi" (1 Timotheo 1:15).
10. (Yohana 6:37) Yesu alisemaje kwa yeyote atakayekuja kwake? _____

    Kwa mfano ungemwambia Mungu, "Mungu mpenzi; Mimi ni mwenye dhambi na nimehukumiwa, ninaamini kwamba Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zangu. Ninaupokea msamaha na sasa namwamini Kristo kama Mwokozi wangu." Ukija kwake kwa njia hii, je, atakusamehe dhambi zako na kukuokoa? **Ndiyo**
11. (Yohana 5:24) Muumini anao nini? _____
12. (Yohana 14:6) Ni vitu gani vitatu ambavyo Yesu hujiita yeye mwenywe? (1) _____

    (2) _____ (3) _____

    "Kuna Mungu mmoja, na mpatanishi mmoja kati ya Mungu na Wanadamu, Mwanadamu Kristo Yesu, aliyejitoa mwenyewe kuwa fidia ya wengi ..." (1Timotheo 2:5-6)
13. (Yohana 19:18) Yesu aliuawa kivipi? _____
14. (Yohana 10:17-18) Je, Yesu hakuweza kujiokoa na hila za waliomchukia? au kwa hiari yake aliyatoa maisha yake kuwaokoa wengine? _____

Copyright © 2018 Prison Mission Association – Kanisa la Neema – Bible Correspondence Fellowship

15. (Yohana 15:13) Kwa nini Yesu Kristo alijitolea mhanga maisha yake kwa ajili yetu? _____

_____

"Kwa sababu Kristo alikufa mara moja kwa ajili ya dhambi, mwenye haki kwa ajili ya wasio haki ili kuwaleta kwa Mungu." (1 Petro 3:18)

16. (Yohana 5:24) Anayesikia na kuamini hataingia _____, bali hubadilika toka _____ kuingia _____.

17. (Yohana 2:19-22) Je, Yesu alitabiri juu ya ufufuo wake kutoka kwa wafu? _____

18. (Yohana 11:25) Ni mambo gani mawili Yesu aliyasema kumhusu yeye mwenyewe? Mimi ni _____

_____

Maandiko yanatabiri mateso na kifo cha Kristo, lakini pia yanatabiri kwamba atafufuka kutoka kwa wafu. Kwa kufufuka kwake aliyashinda mauti. Wote wanaoamini wanaokoka kutoka kwenye kifo cha kiroho, na kupata uzima wa milele katika yeye.

19. (Yohana 20:25 na 20:29) Wanafunzi wake walikuwa mashahidi wake wa kuona kwamba Kristo yu hai sasa. Yesu alisema nini kwa wale ambao hawakumwona lakini bado walimwamini? _____

20. (Yohana 20:31) Kwa nini Yohana aliandika mambo haya katika kitabu hiki? _____

_____

21. (Yohana 10:28) Je, uzima wa milele ni zawadi ya bure? au ni kitu ambacho mtu anaweza kukifanyia kazi na kukipata? _____

JAMBO LA KUTAFAKARI

"*Maana mshahara wa dhambi ni mauti, bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Yesu Kristo Bwana wetu"* (Warumi 6:23).

Je, umeipokea zawadi hii? Ndiyo/hapana

KIFUNGU CHA KUKARIRI

Yohana 3:16

SEHEMU YA PILI

Sehemu hii inafundisha Injili (habari njema) ya Neema ya Mungu ikionesha mpango wa wokovu.

1. (Warumi 3:10-11) Taja sifa tatu za kila mwanadamu.
   (1) _____
   (2) _____
   (3) _____
2. (Warumi 3:14-18) Ni mambo gani mengine yanayoeleza hali ya kila mwanadamu?
   (1) mstari 14 - _____
   (2) mstari 15 - _____
   (3) mstari 16 - _____

Copyright © 2018 Prison Mission Association – Kanisa la Neema – Bible Correspondence Fellowship

(4) mstari 18 - _____

3. (Warumi 3:19) Mungu alileta sheria (torati) ili ulimwengu wote uwe _____
4. (Warumi 3:20) Kwa njia ya sheria tunatambua nini? _____
5. (Warumi 3:23) Mungu anasema nini kuhusu wanadamu wote? _____

_____

6. (Warumi 5:8) Mungu aliandaa njia gani kwa ajili ya sisi kuokoka? _____
7. (Warumi 5:10) Tulikuwa adui wa Mungu, lakini tuliweza kupatanishwa na Mungu. Je, hii inawezekanaje? ____

_____

Kumbuka: Upatanisho hufafanua makusudi ya kifo cha Kristo msalabani. Mtu wa asili hupingwa na Mungu na kutengwa naye. Kifo cha Kristo msalabani ilikuwa dhabihu kuu. Ilitupatanisha sisi na Mungu, ilitufanya tukubaliwe naye. Tunapompokea Kristo kama mwokozi wetu, hatuendelei kuwa na doa la dhambi bali tunaoshwa na damu ya Kristo. Tunakuwa viungo katika mwili wa Kristo.

8. (Warumi 6:23) Nini mshahara wa dhambi? _____ Nini zawadi (karama) ya Mungu? _____
   Kumpitia nani zawadi hii hutujia? _____
9. (1 Timotheo 1:15) Ni usemi gani wa imani katika mstari huu? _____

_____

10. (1 Wakorintho 15:3-4) Vifungu hivi hutupa msingi wa ukweli wa injili ambayo Paulo aliihubiri. Andika vifungu hivi kwa maneno yako mwenyewe. _____

_____

11. (2 Wathesalonike 1:8) Kisasi na hukumu vitakuja juu ya watu gani? _____

_____

12. (2 Wathesalonike 1:9) Adhabu ni nini? _____

_____

13. **(**Ufunuo 20:15) Ni nini hukumu ya mwisho kwa waliomkataa Kristo? _____
14. Katika swali la nane tuliona uzima wa milele ni zawadi ya Mungu. Habari hii inakubaliana na habari gani ya Waefeso 2:8? _____
15. (Waefeso 2:8-9) Tunaokolewa kwa neema, na ni kwa njia ya _____
16. (Warumi 5:1) Tunapomwamini Kristo na kuhesabiwa haki, tuwe na nini? _____
17. (Warumi 8:35-39) Kitu gani ni chenye uwezo wa kututenga na upendo wa Kristo? (Zungushia jibu sahihi.)

    (1) Dhiki (2) Shida
    (3) Kifo (4) Hatari
    (5) Mateso (6) Hakuna

18. (Warumi 10:13) Mungu alituahidi nini? _____
19. (1 Timotheo 2:5) Nani ni mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu? _____
20. (1 Timotheo 2:6) Bwana Yesu alifanya nini kwa wote? _____

KIFUNGU CHA KUKARIRI

Warumi 5:8

Copyright © 2018 Prison Mission Association – Kanisa la Neema – Bible Correspondence Fellowship

SEHEMU YA TATU

Katika sehemu ya pili tulikuwa na vifungu vingi kuhusu mpango wa Mungu juu ya wokovu. Baada ya kumpokea Kristo kama mwokozi, sasa tunahitaji kuzijua Baraka tunazopata na marupurupu au baraka tulizo nazo kama watoto katika familia ya Mungu.

1. (Yohana 1:12) Wale waliompokea Kristo wamepewa uwezo wa kuwa nini? _____
2. (Yohana 3:7) Yesu alisema ni lazima mtu afanye nini ili awe mtoto katika familia ya Mungu? _____

   _____

   Katika Yohana 3:5-8 wote ambao wamezaliwa mara ya pili wamezaliwa kwa _____
3. (Wagalatia 4:6) Mungu amefanya nini kwa kuwa sisi ni wana wake? _____

   _____
4. (Warumi 8:16) Roho Mtakatifu hushuhudia pamoja na roho zetu kwamba: _____
5. (Waefeso 4:30) Mungu amefanya nini kutuhakikishia kuwa sisi ni watoto wake? _____

   _____
6. (Waefeso 1:5-7) Tunasoma kwamba tunakubaliwa katika mwanawe mpendwa (Kristo, Mwana wa Mungu).

   Katika mstari wa saba, ni mambo gani mawili tunayopewa pia kwa sababu tumo ndani ya Kristo?

   (1) _____ (2) _____
7. (Waefeso 2:19) Waumini wamo katika kundi lipi la watu? _____
8. (1 Wakorintho 6:11) Mungu amefanya mambo gani matatu kwa ajili ya Wakristo?

   (1**)** _____ (2) _____ (3) _____

   Kumbuka: Maana ya neno *"kutakaswa"* ni "kuwekwa kando kwa ajili ya Mungu," au "kuwekwa kando kwa ajili ya matumizi ya Mungu." Hivyo katika mstari huu tulisafishwa dhambi na kuwekwa kando kwa ajili ya Mungu – yaani tulitakaswa. Mtu aliyetakaswa anaitwa "mtakatifu." Katika Biblia waumini wote ni "watakatifu."
9. (Waebrenia 10:10) Mungu hututakasaje? _____

   _____
10. (1 Wakorintho 6:11) Hapa tunapata maneno *"kuhesabiwa haki"*, yaani hali ya kutangazwa haki na Mungu.

    Kulingana na Warumi 3:24, tunahesabiwaje haki? _____
11. (Warumi 3:28) Tunahesabiwa haki kwa _____ pasipo (mbali na) _____
12. (Warumi 4:5) Maneno gani yanaonesha kwamba hatuwezi kuhesabiwa haki kwa njia ya matendo? _____

    _____
13. (Warumi 4:3) Kwa nini Ibrahimu alihesabiwa haki? _____
14. (Warumi 8:1) Kifungu hiki kinasema nini juu ya wale walio ndani ya Yesu Kristo? _____

    _____
15. (Warumi 8:2) Roho wa uzima katika Kristo Yesu ametuweka huru mbali na _____
16. (Yohana 5:24) Waumini hawataingia _____, bali wamepita kutoka _____

    kuingia _____
17. (Warumi 8:35, 38-39) Tunasoma kuwa vitu vyote vilivyotajwa haviwezi kututenga na nini? _____
18. (1 Wakorintho 6:19) Tumeona kwamba Roho Mtakatifu hukaa ndani ya kila muumini. Kwa hiyo,

Copyright © 2018 Prison Mission Association – Kanisa la Neema – Bible Correspondence Fellowship

mwili wako ni _____

19. (1 Wakorintho 6:20) Tunapaswa kumtukuza Mungu katika miili yetu na roho zetu kwa sababu sisi _____

20. (1 Petro 1:18-19) Bei gani ililipwa kwa ajili ya roho zetu? _____

Tulikombolewa — namna gani napenda kuutangaza!
Tulikombolewa kwa damu ya Mwanakondoo;
Tulikombolewa kwa rehema isiyo na mwisho,
Mtoto wake, na milele ni mimi.
Kimeandikwa na Fanny J. Crosby

KIFUNGU CHA KUKARIRI

Warumi 8:1

SEHEMU YA NNE

Sehemu hii ina vifungu vingi kuhusu Biblia; kwa nini Biblia ni yenye ukweli, na kwa nini ni muhimu kwetu kujua yale inayoyasema. Biblia inaitwa "Neno la Mungu," pia inajulikana kwa jina "Maandiko."

1. (Yohana 17:17) Yesu alisema nini kuhusu Neno la Mungu? _____
2. (Yohana 10:35) Bwana pia alisisitiza kwamba hakuna kosa kabisa ndani ya Biblia kwa kusema _____ _____
3. (1 Thesalonike 2:13) Waumini hawa walimsikiliza Paulo akihubiri. Walipokeaje neno? _____ _____
4. (Warumi 10:17) Ili tupate imani, lazima tusikilize nini? _____
5. (1 Petro 1:23) Tumefanya nini kwa neno la Mungu lidumulo? _____
6. (1 Petro 1:25) Neno la Bwana lafanya nini? _____
7. (1 Petro 2:2) Tutahitaji nini ili tukue kiroho? _____
8. (Matendo 17:11) Wale ambao Paulo aliwahubiria walipokea neno kwa moyo. Halafu walifanya nini? _____ _____
9. (Matendo 20:32) Ni nini liwezalo kutujenga katika maarifa ya kiroho? _____
10. (2 Timotheo 3:15) Maandiko matakatifu yanaweza kutufanyia nini? _____
11. (2 Timotheo 3:16) Tunajua kwamba Mungu aliwafanya watu waandike maneno aliyotaka yaandikwe kwa sababu sehemu ya kwanza ya mstari huu inasema _____
12. Mstari ule ule unaorodhesha mambo manne yaliyo faida ya Neno la Mungu:
    (1) _____ (2) _____
    (3) _____ (4) _____
13. (2 Petro 1:21) Kifungu hiki kinaonyeshaje kwamba Maandiko matakatifu yatoka kwa Mungu? _____ _____
14. (Waefeso 6:17) Neno la Mungu linaitwa _____
15. (1 Wakorintho 15:3-4) Mtume Paulo kila mara aliyanukuu maandiko kuthibitisha ukweli wa Injili aliyoihubiri. Ni mambo gani matatu yalitokea "kama yanenavyo maandiko"?
    (1) _____ (2) _____

Copyright © 2018 Prison Mission Association – Kanisa la Neema – Bible Correspondence Fellowship

(3) _____

16. (Warumi 4:3) Hiki ni kifungu kilichonukuliwa kutoka Maandiko ya Agano la Kale. Kwa nini Ibrahimu alihesabiwa haki? _____

17. (Waefeso 1:13) Kifungu hiki kinasema mara unapolisikia neno la kweli na kuamini, wewe unafanyiwa nini?

_____

18. (Warumi 15:4) Sababu mbili za kuandikwa kwa Maandiko Matakatifu ni:

(1) _____

(2) _____

19. Katika Agano Jipya Neno la Mungu linatoa majina mbalimbali. Baadhi ya haya ni:

(1) Wafilipi 2:16 Neno la _____

(2) Matendo 13:26 Neno la _____

(3) Wakolosai 3:16 Neno la _____

(4) Warumi 10:8 Neno la _____

(5) 2 Wakorintho 5:19 Neno la _____

Umemkaribisha Kristo katika maisha yako kuwa Mwokozi wako? NDIYO / HAPANA

Jichunguze. Unategemea nini ili uokolewe:

_____ (1) Ushirika katika Kanisa? _____ (2) Ubatizo?

_____ (3) Kutii amri kumi? _____ (4) Kufanya matendo mazuri?

_____ (5) Kristo pekee?

KIFUNGU CHA KUKARIRI

Zaburi 119:11

SEHEMU YA TANO

Sehemu iliyotangulia tuliangalia vifungu vinavyotufundisha kuhusu wokovu, Neno la Mungu, na nafasi yetu kama watu waliohesabiwa haki na kutakaswa kuwa wana wa Mungu. Sehemu hii inahusu zaidi mwenendo wa Mkristo na maisha ya kikristo. Mungu ametuwezesha kuishi kwa mapenzi yake na kuzishinda dhambi katika maisha yetu.

Mambo mawili muhimu ambayo ni lazima kila Mkristo ajue ni:

- Kwa kuwa amezaliwa kiroho, sasa amekuwa kiumbe kipya, na
- Upya huu wa maisha unashindana na utu wa kale ambao mara nyingi unatambulika kwa jina “mwili.”

1. (Warumi 7:18) Paulo alisema nini kuhusu mwili? _____

2. (Warumi 8:7) Mambo gani mawili yanatajwa kuhusu nia ya mwili?

(1) _____ (2) _____

3. (2 Wakorintho 5:17) Asili mpya ya muumini wakati mwingine huitwa “kiumbe kipya.” Nini matokeo ya kuwa kiumbe kipya katika Kristo? _____

4. (Wagalatia 2:20) Mtu mpya ni maisha ya Kristo ndani ya muumini. Kama Paulo alivyosema, *“...Kristo huishi ndani yangu.”* (1 Yohana 4:4) Hali hii ya Kristo kuishi ndani yetu hutusaidia kushinda utu wa kale kwa sababu

Copyright © 2018 Prison Mission Association – Kanisa la Neema – Bible Correspondence Fellowship

gani? _____

5. (Waefeso 4:24) Inasema nini kuhusu kiumbe hiki kipya (utu mpya)? _____

_____

6. (Waefeso 4:25-31) Kwa kuwa tumekuwa viumbe vipya katika Kristo, tunaambiwa mambo ambayo hatutakiwi kuyafanya. Mambo haya ni mambo gani?

   (1) (mstari 25) _____

   (2) (mstari 28) _____

   (3) (mstari 29) _____

   (4) (mstari 30) _____

   (5) (mstari 31) _____

7. (Warumi 12:2) Hamu ya Mungu ni kwa ajili yetu kutofuata namna ya dunia hii, bali anataka tufanye nini? _____

_____

8. (Tito 2:11-12) Mstari wa 12 unatufundisha nini kuhusu jinsi tunavyoweza kuishi? _____

_____

9. (Wagalatia 5:19-23) Aya hii inapinga kazi za mwili kwa njia ya kazi ya Roho Mtakatifu ndani yetu. Orodhesha vitu tisa ambavyo ni kazi ya Roho mtakatifu (mistari 22-23):

   (1) _____ (2) _____ (3) _____

   (4) _____ (5) _____ (6) _____

   (7) _____ (8) _____ (9) _____

10. (Wagalatia 5:14, soma Marko 12:31, Warumi 13:9-10) Vifungu hivi vinaeleza umuhimu wa kumpenda jirani yako. Kwa nini upendo ni muhimu? _____

_____

11. Mara nyingi maisha ya kikristo au ya maadili mema huitwa “mwenendo.” Katika vifungu vifuatavyo tunapaswa kuenendaje au kuishije?

    (Wagalatia 5:25) _____

    (Warumi 13:13) _____

    (2 Wakorintho 5:7) _____

    (Waefeso 5:2) _____

    (Wakolosai 1:10) _____

12. (Wagalatia 5:16) Tukitembea kwa Roho, kuna matokeo gani? _____

13. (Waefeso 6:10) Tutapata wapi nguvu kwa ajili ya kupambana na dhambi na Shetani? _____

14. (Wakolosai 3:17) Kifungu hiki husema nini kwa lolote tufanyalo? _____

15. (Wakolosai 3:22-24) Mtume Paulo anaeleza mapenzi ya Mungu kwa watumwa (au walioajiriwa). Kutokana na mstari wa 23 tunapaswa kuwa na tabia gani katika kazi zetu? _____

_____

16. (Wakolosai 4:2) Kifungu kinatuambia nini kuhusu kuomba? _____

_____

17. (1 Wathesalonike 4:3) Ni nini mapenzi ya Mungu juu maisha ya mwili? _____

_____

Copyright © 2018 Prison Mission Association – Kanisa la Neema – Bible Correspondence Fellowship

18. (Warumi 12:19) Kwa nini hatutakiwi kulipiza kisasi? _____
19. (2 Wakorintho 6:14) Maksai hufungwa kwa nira pamoja ili wafanye kazi kama timu moja. Kwa nini tusifungiwe nira pamoja na wasioamini? _____
    _____
20. (2 Wakorintho 5:20) Kwa sababu Kristo ametupatanisha na Mungu, tunapaswa kuwa na hamu kupatanisha wengine naye. Katika kazi hii tunaitwa _____

Tumia nafasi hii kuandika maswali au maoni yoyote uliyo nayo:

_____

_____

_____

_____

_____

_____

Rudisha somo hili kwa:

_____ Namba yetu ya simu_____

_____

_____

Habari zako:

Tarehe: _____ Jina lako:_____

Anwani yako: _____

Mji: _____Namba yako ya Simu:_____

Copyright © 2018 Prison Mission Association – Kanisa la Neema – Bible Correspondence Fellowship